# EAST AFRICAN BREWERIES PLC

## FOMU YA UWAKILISHI

MIMI/SISI: ______________________________________________

Akaunti ya Hisa Nambari ______________________________________________

Wa (Anwani) ______________________________________________

Nikiwa/tukiwa mwanachama/wanachama wa East African Breweries PLC, namteua/tunamteua:

______________________________________________

Na asipopatikana, Mwenyekiti wa Mkutano aliyeteuliwa, kuwa mwakilishi wangu/wetu na kupiga kura kwa niaba yangu/yetu katika Mkutano Mkuu wa Kila Mwaka wa Kampuni utakaoandaliwa Alhamisi, 12 Septemba 2024 na tarehe nyingine yoyote iwapo utaahirishwa.

Kama shahidi/mashahidi Naweka saini /Tunaweka saini leo tarehe ____________ ya mwezi wa ______________________ 2024.

Saini ______________________________ Saini ______________________________

Tafadhali weka alama vyema kwenye kijisanduku hapa chini kumuelekeza mwakilishi wako/wenu jinsi ya kupiga kura

| Azimio | | Kuunga | Kupinga | Kususia |
|---|---|---|---|---|
| 1) | Kupokea, kutathmini na kuidhinisha Taarifa za Kifedha Zilizokaguliwa za mwaka uliokamilika mnamo 30 Juni 2024 pamoja na ripoti za Mwenyekiti, Wakurugenzi na Wakaguzi wa Hesabu zilizomo. | | | |
| 2) | **Mgawo wa faida**<br>a) Kuthibitisha mgawo wa faida wa muda kwa ajili ya Mwaka wa Kifedha uliokamilika 30 Juni 2024, wa Kshs 1.00 kwa kila hisa ya kawaida, uliolipwa baada ya kutozwa kodi ya zuio au withholding tax, mnamo au karibu na 28 Aprili 2024 kwa wenyehisa waliokuwa wamesajiliwa kufikia kufungwa kwa shughuli za kibiashara 16 Februari 2024.<br>b) Kuidhinisha mgawo wa faida wa mwisho wa Kshs 6.00 kwa kila hisa ya kawaida kwa Mwaka wa Kifedha Uliokamilika 30 Juni 2024, ambao utalipwa baada ya kutozwa kodi ya zuio au withholding tax, kama ilivyopendekezwa na Wakurugenzi. Mgawo huo wa faida utalipwa mnamo au karibu na 28 Oktoba 2024, kwa Wenyehisa watakaokuwa kwenye Sajili ya Wanachama kufikia kufungwa kwa shughuli za kibiashara mnamo 16 Septemba, 2024. | | | |
| 3) | Kuchaguliwa kwa wakurugenzi:<br>a) Martin Oduor-Oteino anastaafu kwa mzunguko kuambatana na Kifungu 117 cha Sheria za Kuundwa kwa Kampuni, na, kwa kuwa anahitimu, anajiwasilisha kuomba kuchaguliwa tena.<br>b) Jimmy Mugerwa anastaafu kwa mzunguko kuambatana na Kifungu 117 cha Sheria za Kuundwa kwa Kampuni, na, kwa kuwa anahitimu, anajiwasilisha kuomba kuchaguliwa tena.<br>c) Paul Deo Makanza aliteuliwa katika mwaka huo kujaza pengo la muda katika Bodi. Anastaafu kuambatana na Kifungu 116 cha Sheria za Kuundwa kwa Kampuni, na, kwa kuwa anahitimu, anajiwasilisha kuomba kuchaguliwa tena. | | | |
| 4) | Kuwachagua Wakurugenzi wafuatao, ambao ni wanachama wa Kamati ya Ukaguzi wa Hesabu & Usimamizi wa Hatari, wachaguliwe kuendelea kuhudumu kama wanachama wa Kamati hiyo, kwa kutegemea kuchaguliwa tena kwa Wakurugenzi waliotajwa katika Ajenda nambari 3 hapa juu: Felix Okoboi; Jimmy Mugerwa; Leo Breen; Ory Okolloh, na Sathish Krishnan. | | | |
| 5) | Kupokea, Kutathmini na iwapo itakubalika, kuidhinisha Ripoti ya Malipo ya Wakurugenzi na malipo ya Wakurugenzi kwa mwaka uliomalizika 30 Juni 2024. | | | |
| 6) | Kuwateua tena PricewaterhouseCoopers (PwC) kuendelea kuhudumu kama Wakaguzi wa Hesabu wa Kampuni kwa mujibu wa Kifungu 721(2) cha Sheria ya Kampuni, 2015 na kuipa idhini Bodi ya Wakurugenzi kuamua malipo yao kwa mwaka wa kifedha unaofuata. | | | |

# SUPPLEMENTARY INFORMATION (CONTINUED)

## FOMU YA IDHINI YA MAWASILIANO YA KIELEKTRONIKI

**Tafadhali jaza kwa HERUFI KUBWA**

Jina kamili la Mwakilishi (Wawakilishi): ____________________

____________________

____________________

Anwani: ____________________

Email Address:

____________________

**Nambari ya Simu**

Tarehe: ____________________

Saini: ____________________

Tafadhali weka alama katika **MOJA** kati ya visanduku vilivyo hapa chini na kuirejesha fomu hii kwa Image Registrars katika S.L.P. 9287- 00100 Nairobi, Ghorofa ya 5, jumba la Absa Towers (zamani ikiitwa Barclays Plaza), Loita Street:

**Idhini ya Kusajiliwa**
MIMI/SISI ninatoa/tunatoa idhini ya kusajiliwa kushiriki katika Mkutano Mkuu wa Kila Mwaka utakaofanyika mnamo 1 2 Septemba, 2024.

**Idhini ya kutumiwa kwa Nambari ya Simu iliyotolewa**
NINGEPENGA/TUNGEPENDA kutoa idhini yangu/yetu ya kutumiwa kwa nambari ya simu niliyoitoa/tuliyoitoa kwa ajili ya kupiga kura katika AGM..

**Maelezo:**

1. Iwapo mwanachama atashindwa kuhudhuria yeye binafsi, Fomu hii ya Uwakilishi inafaa kujazwa, kutiwa saini na kutumwa kupitia barua pepe kwa eabl.agm@eabl.com au iwasilishwe (pamoja na barua ya idhini ya wakili au mamlaka nyingine (iwapo itakuwepo) ambayo imetiwa saini chini yake au nakala ya cheti cha kutoa idhini au mamlaka ambacho kimetiwa muhuri) kwa Image Registrars Limited, Ghorofa ya 5, jumba la Absa Towers (zamani ikiitwa Barclays Plaza), Loita Street, S.L.P. 9287-00100 GPO Nairobi ili ipokelewe kabla ya Jumanne 10 Septemba, 2024 saa tano asubuhi (11:00 a.m.), yaani si chini ya saa 48 kabla ya wakati wa kufanyika kwa mkutano au iwapo utaahirishwa au, iwapo kura itapigwa baada ya tarehe ya kufanyika kwa mkutano, au baada ya mkutano ulioahirishwa, sio chini ya saa 24 kabla ya wakati uliowekwa wa kura kupigwa ambayo hupigwa zaidi ya saa 48 baada ya kufanyika kwa mkutano au mkutano ulioahirishwa.

2. Iwapo anayeteua mwakilishi ni kampuni au shirika, Fomu ya Uwakilishi inafaa kupigwa mhuri rasmi wa kampuni au kuidhinishwa na afisa au wakili aliyeidhinishwa kuiwakilisha kampuni au shirika hilo.

3. Kama mwenyehisa, una haki ya kumteua mwakilishi au wawakilishi wa kutekeleza haki zako zote au baadhi ya haki zako kama mwenyehisa na kuzungumza na kupiga kura kwa niaba yako katika mkutano. Uteuzi wa Mwenyekiti kama mwakilishi umetolewa kama njia moja ili kurahisisha mambo. Ili kuteua mtu mwingine kuwa mwakilishi, piga kalamu maneno ‘Mwenyekiti wa Mkutano aliyeteuliwa” na uandike majina kamili ya mwakilishi wako katika nafasi iliyotolewa. Mwakilishi sio lazima awe mwenyehisa wa Kampuni.

4. Kujazwa na kuwasilishwa kwa fomu ya uwakilishi hakutakuzuia wewe mwenyewe kuhudhuria na kupiga kura mkutanoni, ambapo, iwapo itafanyika, kura itakayopigwa na mwakilishi wako haitahesabiwa.

5. Chaguo la “kususia” limeorodheshwa kwenye sehemu ya kupiga kura kwenye fomu hii ya uwakilishi. Matokeo ya kisheria ya kutumia chaguo hili kwenye azimio lolote ni kwamba utahesabiwa kama mtu ambaye hakupigia kura azimio hilo. Idadi ya kura zilizosusiwa, hata hivyo, itahesabiwa na kurekodiwa, lakini hazitatumiwa katika kuhesabu idadi ya kura zilizounga mkono au kupinga kila azimio.